Toleo 97 - Shaaban 1446 H / Februari 2025 M

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Chini ya Urasilimali Utunzaji wa Afya huwa kama Fadhila tu wala Hauchukuliwi kuwa ni Haki Msingi

**HABARI NA MAONI**
Waislamu Lazima Wasimame Pamoja Dhidi ya Maadui wa Uislamu

**MATOLEO**
Wito kwa Waislamu kwa Jumla, na kwa Watu wa Ash-Sham Hasa

**JIBU LA SWALI**
Biashara ya Mtandaoni (E-Commerce)



بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi ya Habari Kenya

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 05/1446 | Alkhamis,17 Jumada al-thani 1446 H | 19/12/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Chini ya Urasilimali Utunzaji wa Afya huwa kama Fadhila tu wala Hauchukuliwi kuwa ni Haki Msingi

Serikali imeanzisha Mamlaka ya Afya ya Kijamii (SHA) ili kusimamia bima ya afya ya jamii nchini. SHA ina hazina tatu za kifedha: Hazina ya Huduma ya Afya ya Msingi, Hazina ya Bima ya Afya ya Jamii na ile ya hali ya Dharura na Ugonjwa hatari. Watoa huduma za afya nchini Kenya wanaweza kuingia katika kandarasi na mamlaka ya SHA ili kutoa huduma za afya kwa walengwa.

Sisi katika Hizb ut Tahrir /Kenya tungependa kueleza yafuatayo:-

Mfumo wa SHA, unaotajwa kuwa unanuia kubadilisha sera ya fedha za afya nchini, unatajwa na serikali kama mfumo ulio bora zaidi kimanufaa kuliko ule wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, (NHIF) uliogubikwa na visa vya rushwa. Hata hivyo, muungano wa mashirika ya Safaricom, Apeiro na Konvergenz Network Solutions Ltd ulishindwa kuwa na mfumo mzuri wa sera za kiutendakazi kuhusiana na SHA. Gharama ya mpango huu wa haraka kama kawaida huanguka kwenye mabega ya walipa kodi ambao tayari wamelemewa na ushuru unaotozwa na utawala usioonyesha huruma.

Katika Mfumo wa Kirasimali, faida ndio kichocheo kikuu cha huduma zozote za sera za kifedha. Kwa msingi huu, kuhama kutoka NHIF hadi SHA kuko mbali kabisa na suala la kuboresha kiwango cha afya cha raia wa kawaida. Hii ni kwa kuwa msukumo mkubwa ni faida ambayo tawala za kibepari zimetanguliza juu ya majukumu yote ya kijamii. Uhalisia huu sio kwa Kenya tu bali ni duniani kote, mfano mzuri ukiwa ni dola kuu leo ya Marekani ambapo wagonjwa wanaohitajia gharama kubwa kwa serikali wamekuwa wakipuuzwa na kuhatarishwa afya zao kwa sababu tu ya uchu wa kampuni za bima ya afya hali inayosababisha vurugu miongoni mwa jamii. Kisa cha karibuni ambacho ni ukweli usiopingika ni kuuwawa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa United Healthcare, Brian Thompson.

Tunasema kwamba maslahi yoyote ya umma ni lazima yatekelezwe na serikali kwani huingia kwenye majukumu yake na hili ni kulingana na maneno ya Bwana Mtume (saw):

«الإِمَامُ رَاعٍ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ»

"Imam/ Kiongozi ni mchungaji na ataulizwa juu ya watu anawaochunga"

Kwa muktadha huu, Uislamu umefanya huduma ya afya kuwa ni jukumu la msingi la Serikali na sio fadhila kwa raia; kwa maana hiyo, ndio Uislamu ukawajibisha kwamba usimamizi wa afya unaangukia serikali pekee. Huduma ya afya ya serikali lazima iwe bila malipo kwa raia wote wa Khilafah, Waislamu na wasio Waislamu. Huduma ya afya lazima iwepo, thabiti na ya viwango vya juu kwa wote.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir**

**Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Waislamu Lazima Wasimame Pamoja Dhidi ya Maadui wa Uislamu

**Habari:**

PESHAWAR, Pakistan - Pakistan katika mashambulizi ya nadra ya anga yalilenga maficho mengi ya washukiwa wa Taliban ya Pakistan ndani ya nchi jirani ya Afghanistan siku ya Jumanne, na kubomoa kituo cha mafunzo na kuua baadhi ya waasi, maafisa wanne wa usalama walisema. (Washington Post)

**Maoni:**

Enayatullah Khwarazmi, msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Taliban, alikanusha madai hayo ya Pakistan na kuchapisha kwenye X (zamani Twitter) kwamba "raia wa kawaida, wengi wao wakiwa wakimbizi wa Waziristan," wameuawa katika shambulizi hilo la anga. Khwarazmi ameongeza kuwa "watoto kadhaa na raia wengine waliuawa shahidi na kujeruhiwa" katika shambulizi hilo.

Shambulizi hilo lilitokea wakati ambapo viongozi wa Taliban walikuwa wakiandaa mikutano pamoja na ujumbe wa ngazi ya juu wa Pakistan, kuashiria kuanza kwa maingiliano kama hayo baada ya kusimama kwa mwaka mzima kutokana na madai ya ugaidi, na Balozi wa Pakistan Sadiq alikuwa katika ziara ya kujenga uhusiano na aliandika kwenye ukurasa wa X. Akisema: "Nimekutana na Waziri wa Mambo ya Nje Amir Khan Muttaqi leo. Tulifanya mazungumzo mapana. Tumekubaliana kufanya kazi pamoja ili kuimarisha zaidi ushirikiano baina ya nchi hizo mbili na pia kwa ajili ya amani na maendeleo katika kanda hii."

Ulafi huu wa amani na maendeleo yaliyofafanuliwa na Magharibi umeupofusha uongozi wa Waislamu katika majukumu yao ya awali na matokeo yake tunashuhudia kumwagika kwa damu ya Waislamu katika kila kona ya dunia. Ikiwa upanga umetolewa kati ya ndugu, hili hutumikia maslahi ya Marekani kwa njia nyingi. Waislamu wanaonekana kutokuwa na umoja kiasi kwamba wazo la kuunganishwa linaonekana kutowezekana. Kujionyesha kwa Magharibi kama mlezi na mwokozi wa ulimwengu, mamlaka pekee yenye akili timamu na iliyosafishwa ambayo inawasimamia washenzi wa dunia, Waislamu wakiwa ndio wanaohitajika zaidi katika vizuizi vyake. Baada ya Marekani kuondoka Afghanistan, na kuunda Serikali ya Taliban, jeshi la Pakistan lilijaribu kuchukua hatua za tahadhari za kujitenga na machafuko yaliyoachwa nyuma na Marekani. Viongozi walijua vyema zaidi juu ya uwongo ambao umeishi na mazimwi ambao wameundwa kulingana na hitaji la wakati huo. Moja ya hatua hizi za ulinzi ilikuwa kuwafukuza karibu wakimbizi 800,000 wa Afghanistan kutoka Pakistan. Wengi wa hawa wameishi hapa kwa miongo kadhaa na walipaona kuwa nyumbani kwao. Wengi walizaliwa hapa.

Wanajeshi wa Pakistan wanatakiwa kukumbuka kuwa wao ni wa nchi ambayo iliundwa kwa jina la Uislamu huku watu wakiacha kila kitu nyuma ili kufikia ardhi ambayo Waislamu wote watakuwa salama. Ardhi hii haikuwa ya kabila lolote. Ufafanuzi huu ulitolewa baadaye kwamba Muislamu aliye upande wa mstari ulionyoshwa ni tofauti na Muislamu aliye upande mwingine. Hapa tunatakiwa kufuta mistari badala ya kuwaondoa watu wasioendana na utaifa. Watu wa Afghanistan na watu wa maeneo ya kikabila ya Pakistan wanaweza kuwa rasilimali kwa jeshi letu. Vita vitatu vya Anglo Afghan hadi 2021 Marekani kuondoka kutoka Afghanistan historia imeona mifano mingi ya nguvu ya watu hawa. Wana wetu katika majeshi ya Pakistan na watu wa Afghanistan wanasujudu mbele ya Mungu mmoja. Haki na majukumu yao yanatokana na Aqida ya Kiislamu, na sio juu ya utaifa. Fikra ya Kitaifa inatokana na eneo unalojitambulisha nalo, au eneo linalokupa ukubali wa kimaandishi, kwa hivyo aina yoyote ya mabadiliko ya kijiografia yanaweza kubadilisha utaifa wako. Hali ya Afghanistan, KPK na hata Balochistan inadhihirisha wazi kwamba mipaka ya Dola za Kitaifa ilishindwa kuvunja mafungamano ya karne nyingi ya ukabila. Kinyume na hayo, ukabila umejidhihirisha kuwa na nguvu zaidi kuliko fungamano la kitaifa. Kulinda ubwana na uadilifu wa kieneo kwa misingi ya maeneo yaliyoainishwa na mwanadamu hubadilisha maana ya kulinda kwa ajili ya Uislamu. Inafafanua upya madhumuni ya kupigana na askari atalazimika kupigana na yeyote ambaye mtawala wa Kirasilimali atamtaka kupigana naye na kumuua. Hata akiwa ni ndugu yake Muislamu aliyesimama upande wa pili wa mstari. Sisi kama Waislamu Ahadi yetu iko kwa Mwenyezi Mungu. Damu, upendo, ardhi na manufaa haviwezi kuchukua mamlaka. Kuna methali ya zamani "Niko dhidi ya kaka yangu. Mimi na kaka yangu dhidi ya binamu yangu. Mimi, kaka yangu, na binamu yangu dhidi ya ulimwengu." Hivi sivyo tulivyo. Sisi ni ndugu katika Uislamu na tunapaswa kusimama kidete dhidi ya adui wa Uislamu.
Askari wa jeshi la Pakistan ni wana na ndugu zetu na tunatimiza jukumu letu kwa kuwakumbusha kufanya lao. Uaminifu na utiifu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (swt) pekee na kwa mtawala anayetabikisha sheria kwa mujibu wa maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt). Khilafah kwa njia ya Mtume (saw) haitaokoa tu maisha ya Waislamu bali itawalingania wengi kwenye Uislamu na itawaletea kheri ya duniani na akhera.

***Endelea... UK 4***

**[وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ]**

“Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya makhalifa wa kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia Dini yao aliyo wapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.” [An-Nur: 55]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Ikhlaq Jehan**

# Wito kwa Waislamu kwa Jumla, na kwa Watu wa Ash-Sham Hasa

Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, na rehma na amani zimshukie Mtume wa Mwenyezi Mungu, na jamaa zake, na maswahaba zake, na wanaomfuata.

Mumejifunza kuhusu matukio yaliyoharakishwa huko Ash-Sham, na hatima ya Bashar, dhalimu wa Ash-Sham, ambaye amekuwa mtu wa kufukuzwa na mkimbizi tangu tarehe 8 Disemba 2024. Mumeona kile ambacho kimekuwa dhahiri juu ya udhalimu wake juu na chini, na jinai za aibu waliyotendwa wafungwa, hata hayawani ardhini hawajatenda chochote kama hayo. Kisha mukatazama jinsi watu walivyosherehekea kuangamia kwa dhalimu mijini, vijijini na mabarabarani, wakimshukuru Mwenyezi Mungu (swt) kwa kuwapa ushindi kwa kuondosha utawala wa dhalimu huyo.

Kisha mumeona na kusikia jinsi Amerika, ikifuatiwa na Uturuki, ilivyowakusanya watawala wa Kiarabu huko Aqaba kujadili jinsi serikali mpya ya Syria inapaswa kuwa: [Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano ya Mawaziri wa Kiarabu walikutana leo, Jumamosi, katika mji wa Jordan wa Aqaba kuhusiana na matukio ya Syria... Uturuki... Marekani... Mwakilishi Mkuu wa Muungano wa Ulaya... na mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Syria.] Taarifa hiyo ilisomeka hivi: (Mikutano hiyo ilijadili njia za kuunga mkono mchakato wa kisiasa wa kina ukiongozwa na Syria “ili kufanikisha mchakato wa mpito kwa mujibu wa Azimio 2254 la Baraza la Usalama...”). Mjumbe wa Umoja wa Mataifa nchini Syria Geir Pedersen alisema wakati wa mkutano wake na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Anthony Blinken, kando ya mikutano ya Aqaba [“tunatarajia kuona dola ya Syria ikijitokeza, kama yenye uwakilishi kamili, isiyo ya kimadhehebu, inayojumuisha watu wote, ambayo inaweza kuleta pamoja sehemu zote za jamii ya Syria” (Al Jazeera, 14/12/2024)]. Baada ya hapo, gazeti rasmi la “Uturuki” lilisema [kwamba Erdogan anaweza kufanya ziara ya “kihistoria” jijini Damascus ndani ya wiki mbili zijazo. Alithibitisha wakati wa mazungumzo yake na waandishi wa habari kwamba nchi yake “itasaidia utawala mpya wa Syria katika kujenga muundo wa serikali”. Aliongeza kuwa anatumai kuwa kuundwa utawala mpya wa Syria unaoongozwa na al-Julani kutapelekea kiwango kipya cha uhusiano wa pande mbili. (Sky News Arabia, 20/12/2024)].

Kisha, wajumbe wa Marekani na Ulaya walikuja Syria katika mikutano na serikali mpya ili kupanga hali hiyo kwa namna ambayo wajumbe hao wanaitaka. Wa mwisho wao, mnamo Ijumaa 20/12/2024, alikuwa ujumbe wa Amerika. Mwishoni mwa mkutano huo, Idara ya Operesheni za Kijeshi nchini Syria ilitoa taarifa kuhusu nukta muhimu zaidi ambazo zilijumuishwa katika mkutano wa kiongozi wake, Ahmed Al-Sharaa pamoja na ujumbe wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ambao ulisema: [Upande wa Marekani ulithibitisha dhamira yake ya kuunga mkono watu wa Syria na utawala mpya wa Syria, na kusimama nao katika kukabiliana na faili zinazosubiriwa na changamoto kubwa, kama vile eneo la kaskazini mashariki mwa Syria, na wajumbe walielezea kuunga mkono hatua zilizotangazwa na utawala mpya wa Syria... Taarifa hiyo iliongeza: “Kwa upande wake, wajumbe walitoa shukrani zao kwa juhudi za utawala mpya katika kuwaachilia huru wafungwa, akiwemo Raia wa Marekani Travis... Taarifa hiyo iliendelea: “Kwa upande mwengine, upande wa Syria ulitoa makaribisho yake kwa ujumbe huo... na kueleza kuwa watu wa Syria wanahitaji msaada mkubwa ili kufikia afueni na ustawi katika ngazi zote, ukitoa wito wa kuondolewa vikwazo vilivyowekwa dhidi yake, na kueleza kuwa watu wa Syria wanasimama kwenye masafa yale yale kutoka kwa nchi na pande zote katika kanda hii bila kuiweka Syria katika hali ya mgawanyiko” (Arabic RT - Arab World News, 20/12/2024)].

Kisha mumeona na kusikia jinsi jeshi la Mayahudi lilivyovamia vijiji vya Golan na Quneitra, na kufanya mashambulizi takriban 600 yakilenga maeneo ya jeshi la Syria, hasa vituo vya anga na mifumo ya ulinzi wa anga, katika operesheni kubwa zaidi ya kuharibu uwezo na zana za kijeshi katika historia ya kisasa, kama ilivyoelezwa kwenye tovuti ya Sky News Arabia tarehe 19/12/2024. Mashambulizi yake yaliendelea ndani ya eneo lisilo na wanajeshi hadi ikafika Mlima Hermon: [“Majeshi ya Israel yalikalia Mlima Hermon walipoingia kwenye eneo lisilo na jeshi kati ya Syria na Milima ya Golan iliyokaliwa kwa mabavu.” (Al Jazeera, 18/12/2024)]. Hivyo basi, baada ya umbile la Kiyahudi kufanya mamia ya mashambulizi dhidi ya vituo vya

***Endelea... UK 5***

kijeshi, kiusalama na kisayansi nchini Syria, mbele ya macho ya watawala wapya wa Syria, watawala wa Waarabu na watawala wa nchi za Waislamu... kana kwamba jambo hilo haliwahusu! Kilicho kibaya zaidi na cha uchungu zaidi ni kwamba serikali mpya ya Syria inatangaza, pamoja na hayo yote, kwamba haikusudii kuwa na mgogoro na umbile la Kiyahudi, wala na Marekani na Ulaya, na kwamba wanaomba amani na kuondolewa kwa vikwazo juu yao, na kusaidiwa katika ujenzi na ujenzi upya... maombi ambayo ni zaidi ya udhalilifu na fedheha:

Asharq Al-Awsat ilichapishwa kwenye tovuti yake tarehe 15/12/2024: [...Ahmed Al-Sharaa alisema mnamo Jumamosi kwamba 'Israel' inatumia visingizio vidogo kuhalalisha mashambulizi yake dhidi ya Syria, lakini aliweka wazi kwamba yeye hana nia ya kuingia katika migogoro mipya, kwani nchi hiyo inaangazia kujijenga upya baada ya kumalizika kwa enzi ya Bashar Al-Assad... Alisisitiza kuwa masuluhisho ya kidiplomasia ndiyo njia pekee ya kuhakikisha usalama na utulivu "mbali na matukio yoyote ya kijeshi yasiyopigiwa hesabu"]. Al-Jazeera imenukuu gazeti la 'New York Times' [Al-Sharaa alizitaka serikali kama vile Marekani kuondoa kibandiko cha kigaidi kutoka kwa Hay'at Tahrir Al-Sham, na pia ametaka kuondolewa vikwazo vyote ili Wasyria waweze kuijenga upya nchi." (Al-Jazeera, 17/12/2024).

Enyi Waislamu kwa jumla, na hasa watu wa Ash-Sham: Utawala mpya wa Syria, unaoongozwa na al-Julani, una uhusiano wa karibu na utawala wa Uturuki unaozunguka katika mzunguko wa Amerika. Ikiwa anadhani kwamba kwa kuifurahisha Marekani, atatabikisha utawala wa kisekula, ataipiga vita Khilafah na walinganiaji wake, na kufunga jela juu yao, ingawa alifungua jela nyengine na kuwaachia huru wote waliomo isipokuwa wanachama wa Hizb ut Tahrir wanaofanya kazi kurudisha utawala wa Mwenyezi Mungu duniani, Khilafah Rashida, na hilo ni ili kuifurahisha Marekani na Magharibi katika vita vyao dhidi ya Khilafah na watu wake. Akiwa anadhania kuwa hili litahifadhi kiti chake (cha utawala), basi amekosea isipokuwa ataendelea kuwatumikia, kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alitufahamisha kupotea kwa mwenye rai hii, kwani yeye (saw) amesema katika yale aliyoyapokea Ibn Hibban katika Sahih yake kutoka kwa al-Qasim kutoka kwa Aisha, Mama wa Waumini, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

«مَنْ أَرْضَى اللهَ بِسَخَطِ النَّاسِ كَفَاهُ اللهُ، وَمَنْ أَسْخَطَ اللهَ بِرِضَا النَّاسِ وَكَلَهُ اللهُ إِلَى النَّاسِ»

"Yeyote anayetaka radhi za Mwenyezi Mungu kwa ghadhabu za watu, Mwenyezi Mungu atamtosheleza kwa watu. Na yeyote anayetaka radhi za watu kwa ghadhabu za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamkabidhi kwa watu."

Yeyote anayeangalia hatima ya wafuasi wa wakoloni makafiri na wale wanaofuata nyayo zao ili kuwafurahisha ataona kwamba hali zao zinazungumza wazi juu ya hatima yao:

[إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ]

"Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia." [Qaf: 37].

Enyi Waislamu kwa jumla na hasa watu wa Ash-Sham: Mfumo pekee alioufanya Mwenyezi Mungu (swt) kuwa ni faradhi na Mtume wake (saw) na Makhalifa waongofu wakautabikisha, ni kuhukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, safi na ya wazi, pasi na dosari yoyote, na bila mfumo mwengine kuchanganywa ndani yake. Kwa hiyo wema hauchanganywi na uovu, na sehemu za Uislamu na sehemu za usekula hazitabikishwa (pamoja). Bali utawala ni kwa mfumo wa Khilafah Rashida bila ya mgawanyiko.

[وَأَنِ احْكُمْ بَيْنَهُمْ بِمَا أَنْزَلَ اللهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ وَاحْذَرْهُمْ أَنْ يَفْتِنُوكَ عَنْ بَعْضِ مَا أَنْزَلَ اللهُ إِلَيْكَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَاعْلَمْ أَنَّمَا يُرِيدُ اللهُ أَنْ يُصِيبَهُمْ بِبَعْضِ ذُنُوبِهِمْ..]

"Na wahukumu baina yao kwa aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao. Nawe tahadhari nao wasije kukufitini ukaacha baadhi ya aliyo kuteremshia Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka, basi jua kwamba hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwasibu kwa baadhi ya dhambi zao …" [Al-Ma'idah: 49]

Mumejitolea muhanga, mumedhurika, wengi wenu wameuawa shahidi na wengi wamejeruhiwa. Mihanga hii lazima iwe ya kusimamisha utawala wa Mwenyezi Mungu (swt) duniani, Khilafah Rashida, na sio kubadilisha serikali moja ya kisekula kwa nyengine, hata kama jina na anwani vinatofautiana. Hivyo, mihanga yenu itakuwa nuru inayomulika Ash-Sham. Walakini, ikiwa mihanga hii itakuongozeni kubadilisha mfumo mmoja ulioundwa na mwanadamu na kuweka mfumo mwengine ulioundwa na mwanadamu, basi mutakuwa mithili ya yule anayefungua uzi wake uliosokotwa baada ya kuwa na nguvu:

[وَلَا تَكُونُوا كَالَّتِي نَقَضَتْ غَزْلَهَا مِنْ بَعْدِ قُوَّةٍ أَنْكَاثاً..]

"Wala msiwe kama mwanamke anaye uzongoa uzi wake baada ya kwisha usokota ukawa mgumu." [An-Nahl: 92]

Enyi Waislamu kwa jumla, na watu wa Ash-Sham hasa: Kiongozi wa Hizb ut Tahrir, asiyewadanganya watu wake, anakuonyeni juu ya mikono ya mashetani wa wanadamu wanaotaka damu yenu imwagike bure, ili msifikie wema msafi na dhahiri, kuhukumu kwa yale yote aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, bali hukmu iliyotungwa na mwanadamu lakini yenye jina na maana tofauti. Badala ya kuwa Umma ambao makafiri wanauchukulia kwa uzito, mumerudi kuwa wafuasi wa makafiri wakoloni na vibaraka wao, na huu ni uhalifu, Mwenyezi Mungu aepushie mbali, ambao hatima yake ni udhalilifu duniani na adhabu kali kesho Akhera.

[سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ]

"Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya." [Al-An'am: 124]

Jihadharini msiipoteze mihanga yenu, hasa kwa vile Ash-

***Endelea... UK 6***

Sham lazima iwe ndio kitovu cha nyumba ya Uislamu, kama alivyotufahamisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) katika Hadithi ambayo At-Tabarani ameipokea katika Al-Mu'jam Al-Kabir kutoka kwa Salamah bin Nufayl, ambaye amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

«عُقْرُ دَارِ الْإِسْلَامِ بِالشَّامِ»

"Kitovu cha nyumba ya Uislamu ni Ash-Sham."

Kwa hivyo fanyeni kila muwezalo kuzuia masuluhisho mabovu ya kisiasa ya kisekula ambayo wakoloni makafiri na vibaraka wao wanataka. Msiruhusu mihanga yenu katika matukio haya ipotee bure na kubakia alama tu!

Na iungeni mkono Hizb ut Tahrir, inayofanya kazi ya kusimamisha utawala wa Uislamu, Khilafah Rashida, na mtapata malipo makubwa na ushindi mkubwa, Mwenyezi Mungu akipenda. Kisha mutakuwa miongoni mwa wanaostahiki bishara njema:

[نَصْرٌ مِنَ اللهِ وَفَتْحٌ قَرِيبٌ وَبَشِّرِ الْمُؤْمِنِينَ]

"Nusura itokayo kwa Mwenyezi Mungu, na ushindi ulio karibu! Na wabashirieni Waumini!" [As-Saf: 13]

**H. 19 Jumada II 1446**
**M. : Jumamosi, 21 Disemba 2024**
**Hizb-ut-Tahrir**

## JIBU LA SWALI

# Biashara ya Mtandaoni (E-Commerce)




**Swali:**

Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh,

Mwenyezi Mungu aubariki wakati wenu, ndugu zangu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,

Nataka kukuulizeni swali na nataraji kupata jibu lenye ufafanuzi wa kina

Swali: Je, biashara ya mtandaoni (e-commerce) na kampuni ya DXN ya Malaysia inaruhusiwa? Kampuni hii inategemea uuzaji wa virutubisho vya lishe, shampoo, krimu za ngozi...nk. Unapo nununua kutoka kwake kiasi fulani, inatoa punguzo (discount). Pindi pointi zako zikifika 100 inakupa punguzo la asilimia sita. Kadiri unavyopata pointi zaidi, ndivyo inavyokupa punguzo kubwa zaidi, na pointi hizi hubadilishwa kuwa kiasi cha pesa ambacho huhamishiwa kwako ama kwa njia ya bahasha au barua ambayo hutolewa kwako kila mwezi, au kuhamishiwa kwenye salio (balance) lako la benki. Nataka kutaja kwamba unaweza kuongeza wanachama kwenye kampuni hii, kila mwanachama anayenunua kutoka kwa kampuni hii anapata pointi, na kwa kurudi unapata pointi kwa sababu mwanachama huyu alisajiliwa kupitia wewe. Bila shaka, unaweza kusajili idadi ya watu unaotaka, na kadiri watu hawa wanavyopata pointi zaidi, ndivyo pointi zako zinavyoongezeka. Kwa hivyo, salio la pesa zilizohamishwa kwako zinaongezeka, na mchakato huu unaendelea kukua hadi uweze kuwa mshirika katika kampuni hii na kupata faida kubwa. (Tafadhali someni kwa makini kuhusu kampuni hii na munipe jibu la kina kuhusu hilo) Shukran

*Endelea... UK 7*

**Jibu:**
Wa Alaikum Assalam Wa Rahamtullah Wa Barakatuh,
Hapo awali dada mmoja alituuliza swali kama hili kuhusu kuamiliana na kampuni ya DXN ya Malaysia, na tulilijibu mnamo 7/11/2024 M. Lina maelezo ya kina zaidi kuliko swali lako. Ninakufikishia swali lililotangulia na jibu letu kwake, na pengine litatimiza lengo, Mwenyezi Mungu akipenda:

**[Swali**: Sheikh wetu mkubwa, Assalam Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuh,
Ninafanya kazi katika kampuni ya Malaysia inayoitwa DXN, ambayo hutengeneza bidhaa za afya na uchunzaji wa kibinafsi. Nilikutana na rafiki mmoja kutoka Jordan na alinisajili katika kampuni hii na kunipa nambari ya uanachama. Niliuliza watu kadhaa kuhusu kazi ya kampuni hii, je ni halali au haram? Wakanijibu kuwa ni halali. Lakini baada ya kuhudhuria mafunzo na mihadhara kuhusu mpango wa fedha, nilianza kuwa na shaka juu ya kazi yake na iwapo kuna chochote cha haram ndani yake?

Kazi ya kampuni hii imeegemezwa juu ya njia mbili za uuzaji:
Njia ya kwanza: Njia ya uuzaji wa moja kwa moja: Ambapo ninanunua bidhaa kwa bei ya jumla na nambari yangu ya uanachama kutoka kwa sehemu za mauzo za kampuni na kuziuza kwa faida yangu mwenyewe, ambapo kampuni hunipa idadi fulani ya pointi kwa kila bidhaa ninayonunua, na nikikusanya pointi 100 au zaidi kila mwezi, inanipa bonasi ya pesa taslim, ambapo asilimia yangu mwanzoni ni 6%, lakini nikikusanya pointi chini ya pointi 100, hainipi pesa, lakini pointi zinabaki katika akaunti yangu binafsi ili kukusanywa kufikia cheo cha wakala nyota.
Njia ya pili ya uuzaji (lakini sikuifikia), ambayo ni: Njia ya masoko ya mtandao wa ngazi mbalimbali: Ambapo timu huundwa na udalali kupigiwa hesabu, ambapo, kwa mfano, Kiongozi S hukusanya timu inayojumuisha S, A, na J, na kila mmoja wa timu ya Kiongozi S anakusanya pointi 100. Kiongozi S hapati faida zake isipokuwa apate pointi 100, na vivyo hivyo, hakuna mtu kutoka kwa timu anayepoteza haki yake.
Udalali kwenye timu ni kama ifuatavyo: Tofauti kati ya asilimia ya kiongozi na asilimia ya mwanachama wa timu huzidishwa kwa 35% huzidishwa kwa idadi ya pointi zilizokusanywa na mwanachama. Pointi zinazokusanywa na mwanachama na timu zinasalia katika akaunti ya jumla ya mwanachama hadi apate cheo cha wakala nyota.
Naomba radhi kwa urefu wa swali na maelezo. Mwenyezi Mungu akulinde ili usimamishe Khilafah Rashida. Natumai nimeliweka swali wazi. Mwenyezi Mungu akubariki na atuongoze sisi na wewe kwa yale anayoyapenda (swt) na kuyaridhia.) Mwisho.
**Jibu**: [Wa Alaikum Assalam Wa Rahamtullah Wa Barakatuh,
Awali ya yote, Mwenyezi Mungu akubariki kwa dua zako nzuri kwa ajili yetu, na tunakuombea kheri.

**1-** Kuhusu njia ya kwanza ya kuamiliana na kampuni hiyo, umesema katika swali kwamba unanunua bidhaa kwa bei ya jumla na kuziuza na kupata faida, na juu ya hiyo, ikiwa unauza asilimia fulani ya bidhaa kulingana na masharti yaliyowekwa na kampuni, unapata faida nyingine kutoka kwa kampuni (cash bonus)... ikimaanisha kuwa kampuni inajifunga kukupa bonasi ya pesa taslim (cash bonus) ikiwa unauza asilimia inayotakiwa ya bidhaa kila mwezi, na hii aghlabu ni kwa ajili ya kuwashajiisha wateja kuongeza maradufu mauzo yao... Ikiwa jambo ni kama tulivyoeleza hapo juu, basi njia hii ya muamala inaruhusiwa kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu kwa sababu kununua bidhaa kwa bei ya jumla na kuziuza kwa faida inajuzu na ni biashara inayojulikana vyema iliyojumuishwa katika maneno ya Mwenyezi Mungu (swt):

**وَأَحَلَّ اللَّهُ الْبَيْعَ وَحَرَّمَ الرِّبَا**

“Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharimisha riba.” [Al-Baqara: 275]

Pia kampuni inaweza kukuahidi kiasi cha pesa ikiwa utauza asilimia fulani ya bidhaa, na hii inachukuliwa kuwa zawadi, na tulitaja katika jibu la swali la tarehe 14/5/2007 M, kuhusu jambo kama hilo, yafuatayo: [Kumpa mtu anayenunua kiasi fulani kiasi cha ziada, zawadi au kitu mithili ya hicho, inajuzu. Uuzaji huo ni halali, na kiasi cha ziada kinaanguka chini ya zawadi, ambayo ni halali.].

Walakini, ruhusa hii ya muamala huu na kampuni ni sahihi kwa masharti mawili:
Kwanza: Kwamba ununuzi wako uwe kwa bei ya jumla kama ilivyo bei ya jumla sokoni, yaani ndani ya mipaka ya bei ya jumla sokoni, na usiivuke kwa njia ambayo inaifanya kufikia kiwango cha ulaghai mkubwa kwa kumnyonya mnunuzi kwa kumdanganya kuwa atapata bonasi ya pesa taslim...nk. Ulaghai umeharamishwa, kama alivyosimulia Al-Bukhari kutoka kwa Abdullah bin Omar (ra) kwamba mtu mmoja alimtajia Mtume (saw) kwamba anadanganywa katika mauzo, hivyo akasema:

**«إِذَا بَايَعْتَ فَقُلْ لَا خِلَابَةَ»**

“Unapouza, sema: ‘Hakuna udanganyifu.’” Khilaba (neno katika Hadith) – lenye kasra kwenye herufi kha – ni udanganyifu. Udanganyifu ni haramu.

Pili: Kwamba njia hii ya muamala iwe huru na njia ya pili iliyotajwa katika swali, yaani ikiwa kuifanyia kazi njia hii ya kwanza iko kando na kuifanyia kazi njia ya pili, lakini ikiwa imeshikamana nayo na ni sharti kwa njia ya pili, basi yale tutakayoyataja kuhusu njia ya pili yatatekelezeka kwake pia.
**2-** Kuhusu njia ya pili ya kuamiliana na kampuni hiyo, kile kilichotajwa katika swali hakiko wazi, lakini inaonekana kuwa hakina tofauti sana na uuzaji wa mtandaoni ulio maarufu, na tumejibu mada ya uuzaji wa mtandaoni katika zaidi ya jibu moja lililotangulia, na tumeonyesha kuwa haijuzu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.

Kutokana na majibu haya, nitakutajia majibu mawili ya maswali yanayofanana na swali lako:
Jibu kwa Swali la tarehe 19/8/2015 M, ambalo linahusu kampuni ya Quest Net, ambayo ni aina ya uuzaji wa

***Endelea... UK 8***

mtandaoni, na haya ndiyo maandishi yake:
[Baada ya kuhakiki uhalisia wa kampuni ya “Quest Net”, na tofauti ya mbinu zake za muamala, ingawa fikra ni lile lile, ambayo ni kwamba kampuni inaamiliana na wauzaji wanaoleta wanunuzi “wateja” kwake, na kuwapa kamisheni (commission) kulingana na masharti fulani, ikimaanisha kwamba wao ni madalali wa kampuni, wanaleta wanunuzi na kuchukua kamisheni kwa ajili yao... Kutokana na kutafakari uhalisia wa muamala huu, yafuatayo yanadhihirika:
Kwanza: Aina hii ya makampuni yanaamiliana na mtandao huu wa masoko katika bidhaa kadhaa, na makampuni haya yanaweka masharti kwamba yeyote anayeuza bidhaa zake anunue baadhi ya bidhaa hizo, na baada ya hapo wanampa haki ya kuleta wateja kwao, na kumpa kamisheni kwa malipo yao (yaani yeye ni dalali wa kampuni ambaye huleta wanunuzi kwake na kuchukua kamisheni kutoka kwa kampuni). Kampuni haitampa kamisheni hadi alete wanunuzi sita kulingana na swali la Asia ya Kati, na hadi alete wawili kulingana na swali la eneo jengine ... yaani kulingana na programu ya kampuni ambayo inaitayarisha kwa kusudi hili. Kwa maana nyengine, mnunuzi wa kwanza anachukua kamisheni kwa wale wawili “au sita” aliowaleta, pamoja na kamisheni nyengine kwa wanne ambao wawili hao wa kwanza waliwaleta, au kwa sita ambao wawili hao wa kwanza waliwaleta.
Na kazi ya uuzaji “udalali” inaendelea kwa njia hii, yaani katika mfumo wa mlolongo wa udalali au mtandao wa uuzaji.
Pili: Aina hii ya biashara ni kinyume na Shariah, na hii ndiyo sababu:
**1-** Kampuni inaeleza kuwa “muuzaji” lazima anunue kutoka kwa bidhaa zake ili awe na haki ya kuifanyia kazi kama dalali kwa ajili ya kamisheni, yaani analeta wateja kwake na kuchukua kamisheni kutoka kwao, iwe kamisheni hiyo ni baada ya kuleta wanunuzi sita au baada ya kuleta wanunuzi wawili.
Hii ina maana kwamba mkataba wa ununuzi na mkataba wa udalali ni mikataba miwili ndani ya mkataba mmoja, au miamala miwili ndani ya muamala mmoja, kwa sababu ni sharti la mmoja kwa mwingine. Haya yameharamishwa, kwani Hadith inasema:

«نَهَى رَسُولُ اللهِ ﷺ عَنْ صَفْقَتَيْنِ فِي صَفْقَةٍ وَاحِدَةٍ»

“Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amekataza mikataba miwili ndani ya mkataba mmoja.” Imepokewa na Ahmad kutoka kwa Abd al-Rahman ibn Abd Allah bin Mas`ud kutoka kwa baba yake. Yaani ni kama nikwambie: Ukiniuzia, nitakuajiri au nitakuwa dalali wako, au nitanunua kwako... nk. Ni wazi kuwa huu ndio uhalisia uliopo kwa mujibu wa swali, kwani uuzaji na udalali viko ndani ya mkataba mmoja, ikimaanisha kwamba ulazima wa kununua kutoka kwa kampuni ni sharti la kazi ya udalali, yaani wa masoko na kamisheni kwa wanunuzi wanaoletwa kwenye kampuni.
**2-** Udalali ni mkataba kati ya muuzaji na yule anayemletea wateja. Kamisheni ya udalali katika mkataba huu inapewa wale ambao mtu huwaleta kwa kampuni, si kwa wale ambao wengine huwaleta. Kwa kuwa kamisheni ya udalali katika muamala uliotajwa hapo juu inachukuliwa na dalali “muuzaji” kwa niaba ya wateja ambao huwaleta kununua kutoka kwa kampuni, na pia kwa niaba ya wale ambao wengine huwaleta, hii ni ukiukaji wa mkataba wa udalali.
**3-** Bei ya manunuzi kutoka kwa kampuni inaambatana na ulaghai mkubwa, na ingawa mnunuzi anafahamu hilo, jambo hilo halikosi hadaa kutokana na mbinu “potofu” zinazotumiwa na kampuni kukuza biashara yake kwa njia ambayo hupelekea mnunuzi kulipa bei kubwa ya bidhaa ya kampuni ambayo haina thamani hata ya sehemu ndogo ya bei halisi... Yote hii ni kwa sababu kampuni inakuza mustakabali (mzuri) wa mnunuzi huyu kwa sababu atapata fursa ya kuitafutia soko bidhaa ya kampuni kwa badali ya kamisheni ya (wanunuzi) anaowaleta kwenye kampuni, pamoja na wanunuzi wanaoletwa na wale aliowaleta kwanza!
Mnunuzi anaposhindwa kuleta wanunuzi, hasa wale walio mwisho wa mlolongo wa wanunuzi, anazungukwa na udanganyifu, na anapoteza bei kubwa aliyolipa kwa bidhaa isiyo na thamani hata ya ushuri moja ya kile alicholipa! Udanganyifu umeharamishwa katika Uislamu. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema:

«...الخَدِيعَةُ فِي النَّارِ»

“Udanganyifu unapelekea Motoni...” Imepokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Ibn Abi Awfa. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) alimwambia mtu mmoja aliyekuwa akidanganywa katika mauzo:

«إِذَا بَايَعْتَ فَقُلْ لَا خِلَابَةَ»

“Unapouza, sema, 'Hakuna udanganyifu.'” Imepokewa na Al-Bukhari kutoka kwa Abdullah ibn Umar (Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili). Khilaba ni udanganyifu. Hii ndiyo maana halisi ya Hadith, maana yake inaashiria kuwa udanganyifu umeharamishwa. Hivyo, muamala huu hauruhusiwi kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu.
Kwa kumalizia, kuamiliana na kampuni ya “Quest Net” kwa namna iliyoelezwa katika maswali ni muamala ambao ni kinyume na sheria ya Kiislamu...] Mwisho wa kunukuu.
Hii ndiyo ninayoiona kuwa rai yenye nguvu zaidi katika jambo hili, na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi zaidi na ni Mwenye Hekima.
Yote haya yanamaanisha kuwa njia ya pili iliyotajwa hapo juu haiendani na sheria ya Kiislamu. 7/11/2024]

Natumai kuwa jibu letu la hapo awali lililotajwa hapo juu litatosheleza.

**Mwenyezi Mungu ndiye Msaidizi.]] Mwisho.**

**Ndugu Yenu**

**Ata Bin Khalil Abu Al-Rashtah**

**17 Jumada Al-Akhira 1446 H**

**19/12/2024 M**